



# 2024 Worldwide Crusade in Honour of the Immaculate Heart of Mary

**Mwaliko kwa Ulimwengu wote wa mapambano ya kiroho kwa Heshima ya Moyo Safi wa Maria kuomba Mungu aingilie kati shida kubwa ya Kanisa**

Huko Fatima, Mama Yetu alitupa sala ya Rozari na ibada ya Jumamosi Tano za Kwanza kama njia nzuri ya kiroho ya kupata upendeleo maalum wa kimungu.

Ibada ya Jumamosi Tano za Kwanza yanajumuisha yafuatayo: Jumamosi ya kwanza ya miezi mitano mfululizo, kupokea sakramenti ya Kitubio na Komunyo takatifu, kusali Rozari, na kutafakari kwa dakika kumi na tano angalau moja ya mafumbo kumi na tano ya Rozari, kwa nia ya kufanya malipizi ya dhambi dhidi ya Moyo Safi wa Maria.

Mbele ya shida na taabu kubwa inayolikumba Kanisa Katoliki sasa, umoja wa chama cha Mama Yetu wa Fatima unaanzisha vita vya kiroho vya dunia nzima vinavyojumuisha sala ya kila siku ya Rozari Takatifu na mazoezi ya Jumamosi Tano za Kwanza, ili kusihia kwa njia ya Moyo Safi wa Maria, msaada wa pekee wa Mungu na , hasa kwa Kiti Kitakatifu huko Roma.

Mpambano huu wa kiroho utanza Jumamosi ya kwanza ya Januari 2024 (Januari 6) na kuhitimishwa Jumamosi ya kwanza ya Desemba 2024 (Desemba 7).

Tarehe 8 Desemba 2023,  
Sherehe ya Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili.

Christopher P. Wendt, Mkurugenzi wa Kimataifa wa Chama cha Bikira Maria, Mama Yetu wa Fatima

+ Athanasius Schneider, Msaidizi wa Kiroho wa Chama cha Bikira Maria, Mama Yetu wa Fatima, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Mtakatifu Maria huko Astana

